



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NANYUMBU



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na. NDC/F.30/1/VOL IV/80


Tarehe: 4 APRILI, 2025.

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC),
SLP 938,
Dar es Salaam.

Yah: **UTAMBULISHO WA KAMPUNI YA VILLAGE CLIMATE SOLUTIONS LIMITED (VCSL)**

Relea somo tajwa hapo juu.

2. Naitambulisha kwako kampuni tajwa hapo juu, ambayo ina malengo ya kuwezesha vijiji mbalimbali hapa Tanzania kutekeleza biashara ya Kaboni kupitia mfumo unaojulikana kama "Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na ukataji miti hovyona uharibifu wa misitu" (MKUHUMI).
3. Mpango huu unasaidia utunzaji wa Misitu ya Asili inayomilikiwa na Vijiji, kwa mujibu wa Vifungu namba 4 (c) (i), 32 (1) (a) na (b) na 35 (6) (b) vya Sheria ya Misitu sura ya 323 ya Sheria za Tanzania.
4. VCSL inashirikiana na vijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu kutekeleza MKUHUMI, kwa lengo la kuzalisha na kuuza kredit za Kaboni, ambapo vijiji vitapata fedha zitakazosaidia maendeleo ya jamii hususani kuboresha kilimo, elimu ya sekondari na ufundi, afya, maji na upatikanaji wa hati miliki za ardhi.
5. Mradi wa VCSL inajulikana kama *Village Climate Solutions Project (VCSP)* na umesajiliwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais na Mfumo wa Kimataifa wa Viwango vya Kaboni (*Verified Carbon Standards - VCS*) na Viwango vya Ubora (*Climate, Community and Biodiversity - CCB standards*) kupitia akaunti namba 1325.
6. Katika Wilaya yetu, Mradi huu unatekelezwa katika kijiji cha Mkumbaru Ramani imeambatishwa.
7. Tunawaomba Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kushirikiana na kampuni hii katika masuala yote yanayohusiana na uwekezaji na utekezaji wa mradi huu ili kuhakikisha mafanikio yake na manufaa kwa jamii.
8. Nawasilisha kwa hatua zako.


MKURUGENZI MTENDAJI (W)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (Halmashauri (W) Nanyumbu), S.L.P 246, Nanyumbu/Masasi, Simu: +255 (023) 2934112/3, Nukushi: +255 (023) 2934114, Barua Pepe: info@nanyumbudc.go.tz Website: www.nanyumbudc.go.tz

